

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA

Simu Na: (026) 2322848, 2321607,
2322853, 2322420,

Nukushi: (026) 2322116, 2322146,
2321013,

Barua pepe: ps@poralg.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:-



Tawala za Mikoa
na Serikali za Mitaa,
S. L. P. 1923,
DODOMA.

Kumb Na. DC 267/507/01/91

27 Desemba, 2016

Makatibu Tawala Mikoa,
TANZANIA BARA

**YAH: MPANGO KAZI WA MATUMIZI YA FEDHA ZITAKAZOTOLEWA
KUPITIA PROGRAMU YA LIPA KULINGANA NA MATOKEO
(PROGRAMME FOR RESULTS - P4R)**

Tafadhali rejeeni kichwa cha barua hii.

Serikali imepokea fedha za kugharamia shughuli za Elimu ya Msingi na Sekondari kupitia Programu ya Lipa kulingana na Matokeo (P4R). Kiasi cha shilingi **22,360,574,170.58** kimeelekezwa kwenye Halmashauri zote nchini.

Katika mwaka huu wa pili wa utekelezaji wa P4R, fedha hizo zinazoelekezwa kwenye Halmashauri zimepatikana katika maeneo matatu (DLR tatu). Maeneo hayo pamoja na asilimia za utekelezaji ni upelekaji shuleni fedha za Ruzuku ya uendeshaji asilimia **89.15** sawa na shilingi **7,738,269,915.00**; upatikanaji wa takwimu ngazi ya shule asilimia **99.99** sawa na shilingi **6,509,551,150**; na uwiano unaokubaliwa wa walimu katika shule za msingi asilimia **41.2** sawa na shilingi **8,112,753,102.58**. Eneo la uwiano wa walimu unaokubalika katika shule za msingi tumefanya vibaya sana. Ili kurekebisha kasoro hizo, fedha hizi zitumike kwa mgawanyo ufuatao:-

1. Asilimia 35 kurekebisha ikama ya walimu ndani ya Halmashauri;
2. Asilimia 30 ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo;
3. Asilimia 25 ukamilishaji wa maabara na madarasa;
4. Asilimia 10 shughuli za P4R ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji.

Aidha, mgawanyo wa fedha hizo kwa Idara ya Elimu ya Msingi na Sekondari uzingatie maeneo yaliyotathminiwa (DLRs). DLR 2.2 (Ruzuku ya uendeshaji) na DLR 3.2 (Takwimu ngazi za shule) zigawanywe sawa sawa kwa Idara zote mbili za Msingi na Sekondari. Fedha zilizotokana na DLR 4.2 (Uwiano wa walimu unaokubalika kishule kwa shule za msingi) zielekezwe kwenye Idara ya Elimu ya Msingi.

Kwa barua hii, tafadhali waelekeze na kuwasimamia Wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wako kuzingatia maelekezo haya kikamilifu. Matumizi ya vifungu hivyo yasibadilishwe.

Eneo la urekebishaji wa ikama kwa walimu wa shule za msingi lisimamiwe kikamilifu na litekelezwe ndani ya mwezi Januari na taarifa iwasilishwe OR-TAMISEMI kabla ya tarehe 15/02/2017.

Fanyeni ufuatiliaji wa karibu wa matumizi ya fedha hizo. Hatua zichukuliwe mara moja kwa yeyote atakayebadili matumizi ya fedha hizi kama yalivyoainishwa katika barua hii.

Taarifa ya utekelezaji iwasilishwe OR-TAMISEMI ikiwa imeunganishwa kimkoa kabla ya tarehe 31/3/2017.

Pamoja na barua hii naambatisha mgawanyo wa fedha hizo (**USD 1 ni sawa na shilingi 2170**).

Nashukuru kwa ushirikiano.



Eng. Mussa I. Iyomba
KATIBU MKUU

Nakala: Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu, Sayansi Teknolojia,
7 Mtaa wa Magogoni,
S.L.P 9121,
11479 DAR ES SALAAM